turathi zisizogusika

UNESCO
United Nations
Educational, Scientific and
Cultural Organization

2005 60 1945

KITENGO CHA TURATHI ZISIZOGUSIKA
www.unesco.org/culture/ich

# TOLEO LA MESSENGER LA TURATHI ZISIZOGUSIKA





FEBRUARI 2006 nº 1
ISSN 2071-7784

## Mataifa Wanachama

KUFIKIA FEBRAURI 15, 2006

1 ALGERIA
2 MAURITIUS
3 UJAPANI
4 GABON
5 PANAMA
6 UCHINA
7 JAMHURI YA AFRIKA YA KATI
8 LATVIA
9 LITHUANIA
10 BELARUS
11 JAMHURI YA KOREA
12 USHELISHELI
13 JAMHURI YA KIARABU YA SYRIA
14 UMOJA WA MILKI ZA KIARABU
15 MALI
16 MONGOLIA
17 CROATIA
18 EGYPT
19 OMAN
20 DOMINICA
21 HINDI
22 VIET NAM
23 PERU
24 PAKISTANI
25 BHUTAN
26 NIGERIA
27 ICELAND
28 MEXICO
29 SENEGAL
30 ROMANIA
31 ESTONIA
32 LUXEMBOURG

## Maafikiano ya Turathi Zisizogusika

### Ni rasmi! Imeidhinishwa na mataifa 30 kwa muda mfupi, Turathi za Tamaduni Zisizogusika zimepitishwa mnamo Aprili 20, 2006.

Siku ya Ijumaa tarehe 20, Januari 2006 ilikuwa ni siku muhimu sana katika kampeni kubwa ya UNESCO inayohusika na kulinda turathi-hai za kidunia.Siku moja, Mjumbe wa Kudumu wa Romania, Mstahiki Andrei Magheru alitoa zana muhimu za kuitikia mwito wa taifa lake kwa Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO, Bw. Koichiro Matsuura ili kulifanya taifa hilo kuwa miongoni mwa mataifa mengine ya ulimwengu yaliyo katika muungano wa kulinda Turathi za Tamaduni Zisizogusika. Kwa kufanya hivyo, Jamhuri ya Romania likawa ni taifa mwanachama la thelathi (30) kujiunga kwenye muungano huo. Tukio hili lina umuhimu wake kama ilivyoelekezwa katika Kifungu cha 34 cha Maafikiano ambacho kinafafanua ya kwamba Maafikiano hayo yataramishwa miezi mitatu tu baada ya taifa mwanachama la thelathini, kupitishwa, kukubalika, na kuidhinishwa. Kufuatia hatua hiyo, Muungano huo utaanzisha rasmi shughuli zake kuanzia tarehe 20, Aprili 2006, ikiwa ni miezi 30 tu baada ya kupitishwa na kikao kikuu cha 32 cha Kongamano la Kuu la UNESCO lililofanyika mwezi Oktoba, 2003. Kwa maneno kutoka kwa kinywa cha Mkurugenzi Mkuu, kukubalika kwa Makubaliano haya na Mataifa Wanachama 8 kutoka bara la Asia, 6 kutoka bara la Uropa, 6 kutoka Uarabuni, 6 kutoka bara la Afrika na mataifa 4 kutoka Latini Amerika, ni ishara kamili kwamba, ''Turathi Zisizogusika zinathaminiwa ulimwenguni kote...na mahitaji yaliyopo ya ulinzi wa kimataifa kwa kuzingatia hali halisi ya kimaisha na masuala ya kiutandawazi". Na wakati kurasmishwa huko kulipoendelea: mwishoni mwa mwezi Januari, mataifa ya Estonia, Luxembourg walileta turathi zao, huku mataifa ishirini zaidi yakitazamiwa kufuata mkondo huo kufikia mwisho wa mwaka wa 2007.

## Tahariri

Kuidhinishwa au kupitishwa kwa Maafikiano ya Turathi za Tamaduni Zisizogusika kunakotarajiwa, itakuwa ni hafla itakayotoa fursa muafaka ya kuzindua *Toleo la Turathi Zisizogusika*. Hata hivyo, zaidi ya kufurahia sherehe hii ya kihistoria, shabaha kamili ya tolea hili itakuwa ni kutoa habari na maelezo ya shughuli za matukio - yaliyopita, yaliyopo na yanayokuja – kusimamia Kitengo kinachohusika na Turathi Zisizogusika cha UNESCO katika ulimwengu mzima. Imetarajiwa kuwafikia wataalamu wa Turathi Zisizogusika pamoja na wahusika wengine, ikiwa ni pamoja na asasi zinazohusiana na UNESCO na mashirika mengineyo ya Umoja wa Mataifa, wajumbe wa mataifa wanachama, tume za kitaifa, mashirika yasiyo ya kiserikali, washirika dau wa kibinafsi na wahusika wengine kutoka kwenye jamii mbalimbali. Tolea hili la *The Messenger* litatoa taarifa za matukio yote yanayohusu kuidhinishwa na kutekelezwa kwa shughuli za Maafikiano hayo. Tolea hilo pia litatoa ripoti ya utafiti na jinsi ambavyo shughuli zinavyoendeshwa nyanjani kwa sasa, namna ya utendakazi, mipango ya vito vyenye thamani na ubora, vito-hai vya wanadamu, lugha zinazohofiwa kuangamia, mila za masimulizi, muziki na densi za kitamaduni, kati ya masuala mengine mengi.
Tunatoa shukrani kwa wanamakala wa – *Calender na Living Heritage News* – angalau wasomaji wetu wameweza kupokea taarifa za makongamano, maadhimisho, machapisho, maonyesho na mabadiliko yanayotokea katika Turathi Zisizogusika (ITH), kama vile mabadiliko yaliyofanyiwa wavuti wetu kwenye mwaka wa 2006.

Ni matarajio yetu kwamba toleo hili litakuwa kifaa muhimu kwa wale wanaochangia moja kwa moja au vinginevyo katika kulinda Turathi-hai za ulimwengu, na tunatarajia kwamba mtatutumia maoni na mapendekezo yenu.

*Rieks Smeets*
*Kitengo cha Turathi Zisizogusika*



© Inst. of Language and Cultural Studies, Bhutan

*Densi ya ngoma ya kinyago kutoka kwa jamii ya Drametse. Kito cha thamani kilichopatikana mnamo mwaka wa 2005. Wachezaji wanaume na wanamuziki wanaowakilisha 'Pacific' na masogora wanaotumbuiza ngoma hii ya vinyago ya kiasili, mara mbili kwa mwaka katika jamii ya Bhutan Drametse.*

KATIKA TOLEO HILI

Mtazama wa Maafikiano uk. 2
Kutoka kwa Kito cha Thamani hadi kwa Orodha Wakilishi ya Vito uk. 2
Nyanjani – Uhabeshi uk. 3
Kalenda uk. 4
Habari za Turathi-Hai uk. 4

*Namna wanavyojionyesha Wajapi katika mazungumzo na uruwaza wao. Hiki ni kito cha thamani kilichopatikana mnamo mwaka wa 2003. Wanachama wa jamii ya Wajapi kutoka Brazil wanatueleza kuhusu maono yao ya ulimwengu kwa kutumia motifu za kijiometrikia, kama zinavyopambwa kwenye miili na vifaa vyao kwa kutumia rangi za majani mbali mbali.*





Photos: © Conselho das Aldeias Waiãpi-Apina

## Mtazamo wa Maafikiano

### Mkutano Mkuu: Halmashauri huru

Wahusika wakuu wa kutoa maamuzi ya Maafikiano, Mkutano Mkuu wa Wahusika Wanachama utafanyika huko Paris, Ufaransa baada ya kipindi cha kila miaka miwili. Mkutano wake wa kwanza umepangwa kufanyika kutoka tarehe 27-29, mwezi Juni mwaka 2006. Kulingana na taratibu zilizopo, Mataifa hayo Wanachama yanafaa kufikisha vyombo vya turathi zao kwa afisi za Mkurugenzi Mkuu, miezi mitatu kabla ya wakati wa mkutano huo mkuu wa kwanza kuweza kufanyika.

### Kamati Maalum kati ya Serikali za Mataifa Wanachama: Utekelezaji na Usimamizi

Kamati Maalum kati ya Serikali za Mataifa Wanachama inayoweka usawa wa kimaeneo ya kijiografia itahusika katika kuyatangaza Maafikiano na kutekeleza maamuzi ya Mkutano Mkuu. Hapo awali Maafikiano haya yalikuwa na Mataifa Wanachama 18 pekee. Wahusika wakuu watateuliwa kwenye kongamano la Mkutano Mkuu utakaofanyika mwezi Juni, 2006, na kufanya kikao chao cha kwanza kabisa hapo mwishoni mwa mwezi wa Septemba 2006. Idadi ya wanachama itaongezwa ili ifike 24 baada ya kuidhinishwa katika Kongamano la hamsini la Maafikiano haya.

### Orodha na Hazina: Muoneko na rasilmali

Vifungu vya 16 na 17 vya Maafikiano vinatoa nafasi za kuwepo kwa orodha mbili. Orodha Wakilishi ya vito vya Turathi za Tamaduni Zisizogusika za wanadamu, Orodha mbadala na ile ya kilimwengu inayofahamika kama Orodha ya Turathi za Kilimwengu, itahakikisha muoneko thabiti wa Turathi za Tamaduni Zisizogusika kote duniani. Wakati huo huo, Orodha ya Turathi za Tamaduni Zisizogusika inayohitaji ulinzi wa haraka zaidi, itawekwa vianzo kamili vya utekelezwaji. Hazina maalum ya kulinda Turathi za Tamaduni Zisizogusika itachangiwa na Mataifa Wanachama na asasi nyinginezo kutoka nje.

### Kufafanua Turathi Zisizogusika

Ufafanuzi wenye utata wa Kifungu cha 2 cha Maafikiano, unaonyesha wazi ya kwamba Turathi Zisizogusika ni kitu kisichoweza kuelezeka kwa urahisi mno. Umechorewa jedwali lifuatalo ili uuelewe ufafanuzi huo kwa wepesi zaidi.

**TURATHI ZA TAMADUNI ZISIZOGUSIKA ZINA MAANA YA:**

**Desturi**

**Mioneko**

**Uwakilishi**

KAMA ILIVYO KATIKA

- mila za uzungumzaji na mwonekano
- muziki wa kitamaduni, densi, na uigizaji
- matendo ya kijamii, mila, sherehe
- Uelewa na mafundisho kuhusu asili na ulimwengu
- Usanii wa kitamaduni

KWA USHIRIKA WA

- Ujuzi na uelewa
- Vifaa na nafasi

KWAMBA

- Jamii na vikundi vya kijamii vinazifahamu kama turathi zao za kitamaduni
- Zinapitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kizazi kingine
- zinabadilika kila wakati
- hutoa nembo na taswira kamili kwa jamii au vikundi vya wana jamii
- huambatana na vyombo vya kimataifa vya mashirika ya haki za kibinadamu.

## Kutoka kwa Kito cha Thamani hadi kwa Orodha Wakilishi ya Vito

### Kuvipongeza vito 90 vya thamani, mradi wa kupokelewa kwa vito vya turathi unamalizika na kualika kuanzishwa rasmi kwa Maafikiano

Tokea kuanzishwa kwake, mradi wa kupokelewa kwa vito vya turathi za Masimulizi na Turathi Zisizogusika za Wanadamu, tayari umefikia idadi kubwa ya nafasi za tamaduni 90 ama mifano ya tamaduni na mioneko inayofahamika kutoka kwa mataifa 69. Kupokelewa kwa turathi za kwanza na pili kulifanyika mnamo mwaka wa 2001 na 2003 mtawalia. Kama inavyoeleza kanuni ya Maafikiano hayo ni kwamba, hakuna mapokezi ya turathi yatakayoendeshwa baada ya kuanzishwa rasmi kwa shughuli za Maafikiano (Kifungu cha 31.3). Mapokezi ya tatu yaliyofanywa wazi kwa umma mnamo tarehe 25, Novemba 2005, yalikuwa ndiyo ya mwisho katika utendakazi wa mradi huu mashuhuri, uliofadhiliwa na Serikali ya Ujapani. Linapotokea ombi kutoka kwa baadhi ya Mataifa Wanachama, Kamati Maalum kati ya Serikali za Mataifa mbali mbali itahusisha turathi hizo katika Orodha Wakilishi ya Vito ya baadae. Kwa sasa, zaidi ya vito na turathi 30 zimehifadhiwa kwenye maeneo ya baadhi ya mataifa wanachama yaliyoidhinishwa. Kama ilivyoelezwa na Mkurugenzi Mkuu mnamo mwezi Novemba 2005, "Tajriba iliyopatikana katika kipindi hiki cha miaka sita ya kutafuta na kupokea vito na turathi za tamaduni zisizogusika, hasa kuhusiana na mbinu za jinsi ya kutambua na kuchagua vito na turathi hizo na pia mafunzo tuliyopata kuhusu mipango ya ulinzi wa miradi inayoendelea kwa sasa, ni jambo ambalo kwa kweli litaingizwa kwenye mabuku ya kihistoria na ambalo litaturahisishia utekelezwaji wa shughuli za Maafikiano haya".

*Wavuti: www.unesco.org/culture/intangible-heritage*





© Anne Damon



© David Stehl/UNESCO

*Muziki na ngoma za kitamaduni za Wahabeshi.*
**Juu kushoto,** *Wachezaji wa Cantor katika sherehe za kidini huku wakicheza kwa tsen-atsel, hali kadhalika wameshikilia vifimbo-cheza vya sala (maqwameya).*
**Juu kulia,** *wanafurahia rindimo la ngoma za kitamaduni kwa kutumia vibanzi vya mbao, katika hafla ya jamii ya Waharari huko jijini Addis Ababa.*

## Nyanjani - Uhabeshi

### Mradi wa miaka minne wa kurekodi tamaduni za muziki na densi zilizopo, umekuwa ndio hatua ya kwanza ya kuboresha uvumbuzi wa kitaifa wa Tamaduni za Turathi Zisizogusika (ICH)

Kuwepo hai kwa zaidi ya lugha 80 na tamaduni za kale zilizodumishwa kwa kupitia misukumo ya mataifa ya Afrika na pia Mashariki ya Kati, Uhabeshi ni taifa lenye uanuwai wa kipekee. Taifa hili limetokana na historia ndefu ya kutengwa na ubadilishanaji uliotokana na hali halisi ya kijiografia na kisiasa ya Uhabeshi ambayo ni ya kipekee. Hali ya uanuwai huo imeakisiwa na kudhihirishwa katika tamaduni za muziki na densi. Ama kwa kweli, muziki wa Kihabeshi umetokana na imani ya Wakristo-Wayahudi (Christian-Orthodox); Uyuda-Uhabeshi (Judeo-Ethipian) ; mila za Kiislamu na hali kadhalika rindimo la muziki wa Kiafrika na namna wanavyopiga ala zao.
Ijapokuwa walipendelea uimbaji wa kutumia sauti, muziki wa Kihabeshi unatumia aina mbali mbali za ala za kimuziki. Baadhi ya ala hizo zinakumbukwa kutoka wakati wa *Agano la Kale*. Miongoni mwa ala zinazofahamika zaidi ni kama; *Baganna na Krar*, kadhalika kuna *fidla ya maseqo*, *ngoma ya kabaro*, na *zumari ya washint*.

Tunashukuru hisani ya Serikali ya Norway, mchangiaji mkubwa wa miradi ya Turathi za Tamaduni Zisizogusika kwa kipindi cha miaka miwili iliyopita, hivi majuzi UNESCO ilizindua mradi wa miaka minne wa kukusanya mila za kimuziki na densi katika taifa zima la Uhabeshi. Kama hatua ya kwanza kwenye ukusanyaji na uvumbuzi wa kitaifa utakaojumuisha Turathi na Tamaduni Zisizogusika za aina mbali mbali, mradi huu utajenga na kuboresha nyenzo na kuweka mifumo thabiti ya uhifadhi wa nyaraka na mila. Ili kuhakikisha kuendelezwa kwa kazi hiyo hata baada ya 2009 na wataalamu wa Uhabeshi, kozi za Muziki-Jamii zitapangwa katika Chuo Kikuu cha Addis Ababa na katika Shule ya Muziki ya Yared kwa kuzingatia mtalaa maalum ulioandikwa kwa Kiingereza na Kihabeshi. Mafunzo ya Uvumbuzi wa Kimuziki yataanzishwa mnamo mwaka wa 2006, kama ''Mandhari ya Kimuziki ya Addis Ababa", na utafiti wa mila mbali mbali za Wahabeshi zinazopatikana katika mji huo mkuu. Kisha wanafunzi wataungana na wataalamu wa Uingereza walio nyanjani, ili kujifunza mila na tamaduni za maeneo tofauti tofauti. Shughuli hizo zinahusisha kufanya utafiti kwenye jamii ya watu wa Maale wanaotoka sehemu ya kusini mwa Uhabeshi na kufanya mipango ya mafunzo na jinsi ya kutumia vyombo vilivyo na uwezo wa kunasa na kurekodi sauti za watu wa Makavazi ya Omo Kusini na pia Kituo cha Utafiti kwenye mji wa Jinka.Vituo mbali mbali na Makavazi katika taifa la Uhabeshi vitapokea mafunzo na vyombo vinavyoambatana na mahitaji yao maalum.

Kufikia wakati wa kukamilika kwa mradi huo hapo mwaka wa 2009, UNESCO itakuwa imekifunza kizazi kipya cha Wahabeshi ili kulibeba jukumu la shughuli za uvumbuzi wa kitaifa wa Turathi za Tamaduni Zisizogusika; kwa kuhusisha viwambo vinginevyo, huku wakitangaza umuhimu wa Turathi za tamaduni Zisizogusika katika mabaraza ya kiwilaya na yale ya kitaifa. Hali hii itachangia moja kwa moja katika kuboresha mbinu za kudumu za Kulinda Turathi-Hai za Uhabeshi. Zaidi ya hayo, kuidhinishwa kwa Maafikiano ya kulinda Turathi za Tamaduni Zisizogusika kunakotegemewa hapo baadae, mradi huu utaliwezesha taifa la Uhabeshi kuyatimiza vyema malengo na azma yake kama Taifa Mwanachama.

*Patum wa Barga.*
*Vito vya thamani vilivyotolewa mnamo mwaka wa 2005. Mara moja kwa mwaka, halaiki ya watu hujaa katika barabara za Barga katika eneo la Catolonia huko Uhispania ili kuhudhuria maonyesho ya vikaragosi vinavyodhihirisha sherehe za kidini zilizosherehekewa miaka mingi iliyopita.*



© Foto Luigi

#### MAELEZO YA MRADI

| | |
|---|---|
| JINA LA MRADI | Uhabeshi: Muziki, densi na ala za kitamaduni |
| MCHANGIAJI | Serikali ya Norway kupitia kwa Hazina ya UNESCO-Norway ya Ushirika inayohusiana na tamaduni. |
| BAJETI | Dola za Marekani $345,388 |
| MUDA WA MRADI | 2005–2009 |
| SHUGHULI | Kuwezesha shughuli za kurekodi huko nyanjani, mbinu za uvumbuzi, maakaba, mafunzo ya sayansi ya Muziki-Jamii |
| ENEO | Uhabeshi kote |
| ANWANI | Afisi za UNESCO za Addis Ababa<br>Bi. Fumiko Ohinata<br>f.ohinata@unesco.org |

MCHAPISHAJI Idara ya Turathi za Tamaduni Zisizogusika (ITH)
Sekta ya Tamaduni, UNESCO
1 Rue Miollis
75732 Paris Cedex 15, Ufaransa
Barua pepe: ich@unesco.org
Kipepesi: +33 (0) 145685752

MHARIRI MKUU Rieks Smeets

JOPO LA UHARIRI Fernando Brugman, Richard Lo Giudice, David Stehl, Reiko Yoshida

MWANA-RUWAZA Jean-Luc Thierry

***Tolea la Turathi za Tamaduni Zisizogusika*** linapatikana katika nakala zilizochapishwa na zile za kielektroniki katika lugha za Kiingereza, Kifaransa na Kihispania.

Matini yote inaweza kuopolewa katika wavuti (www.unesco.org/culture/ich) na kuchapishwa bila malipo ikiwa tu utataja shirika husika.


© Conselho das Aldeias Waiãpi-Apina

# turathi zisizogusika

## KALENDA

**FEBRUARI 7–8** Mkutano: "Mbinu mpya kuhusu uanuwai wa kitamaduni: Jukumu la Jamii". Havana, Cuba.

**FEBRUARI 9** Mkutano wa habari kuhusu Turathi za Tamaduni Zisizogusika wa Wawakilishi wa Kudumu na Wachunguzi wa UNESCO. UNESCO, Paris.

**FEBRUARI 15–17** Warsha: "Kujifunza kutokana na tajriba ya hivi majuzi na kuanza kugundua mafundisho ya kulinda Turathi za Tamaduni Zisizogusika huko Viet Nam". Hanoi, Viet Nam.

**FEBRUARI 9–23** Maonyesho ya picha: Sauti za Andes. UNESCO, Paris.
Chapisho: Sauti za Andes, UNESCO Kuchapisha, Paris, 2006, 80 pp.
ISBN 92-3-204025-5
(Kwa Kifaransa pekee), Yuro 8.

**FEBRUARI 22** Sahihi ya Mkataba kati ya UNESCO na Serikali ya Peru kuhusu kuanzishwa kwa CRESPIAL, Kituo cha Kieneo cha kiwango cha II huko Cuzco (Peru), ili kulinda Turathi za Tamaduni Zisizogusika katika Latini Marekani.

**MACHI 13-15** Mkutano wa Wataalam: "Kuhusika kwa jamii katika kulinda Turathi za Tamaduni Zisizogusika". Tokyo, Ujapani.

**APRILI 18** Sherehe ya Kutuzwa: Tuzo la Sheikh Zayed (UAE), litakalotuza vito vya thamani viwili vilivyopatikana mnamo mwaka wa 2005. UNESCO, Paris.

**APRILI 19–21** (sio tarehe kamili) Mkutano wa Wataalam: "Ufanisi wa Kuvumbua Vito vya Thamani vya Uzungumzaji na pia Turathi Zisizigusika za Kibinadamu". UNESCO, Paris.

**JUNE 27–29** Kikao cha kwanza cha Mkutano Mkuu wa Mataifa Wanachama kuhusu Turathi za Tamaduni Zisizogusika. UNESCO, Paris.

**SEPTEMBA ILIYOPITA** Mkutano wa kwanza wa Kamati maalum kati ya Serikali za Mataifa Wanachama ya kulinda Turathi za Tamaduni Zisizogusika. Eneo la mkutano litatangazwa baadae.

Kwa taarifa zaidi wasiliana nasi kupitia: ich@unesco.org

## HABARI ZA TURATHI-HAI

### Hatua ya Kilimwengu ya Turathi za Utamaduni Zisizogusika ilidhinisha maafinikiano hayo (2003-2006)

Tokea kuidhinishwa kwa Maafikiano hayo mnamo Oktoba mwaka wa 2003, Turathi za Tamaduni Zisizogusika zimejitahidi ili kutimiza malengo mawili makuu: kuhimiza Mataifa Wanachama kuidhinisha Maafikiano hayo na kutayarisha utekelezaji wake kwa kipindi kijacho. Zaidi ya shughuli za usambazaji habari, kabrasha ya 'Swali Linaloulizwa Mara kwa Mara (FAQ)' na kukusanya data ya Turathi za Tamaduni Zisizogusika ulimwenguni kote (ICH), ITH iliandaa mikutano saba ya kimaeneo kwa niaba ya Mataifa Wanachama. Hata hivyo, msururu wa mikutano tisa ya wataalamu, kila mkutano ulikuwa na azma yake maalum, kuibua hoja za kimsingi ambazo zitakuwa na umuhimu mkubwa katika utayarishaji wa maelekezo ya kiusimamizi ya Kamati itakayoshughulikia serikali kati ya mataifa mbali mbali. Mitatu kati ya mikutano hii ya wataalam ilijenga msingi thabiti wa muongozo unaotarajiwa kuundwa ili kulinda viwambo maalum vya ICH. Wakati palipokuwa na zile sherehe za baada ya miaka miwili za mwisho, wafanyikazi wa ITH walialikwa ili kuzungumzia kuhusu Mkataba huo katika zaidi ya maadhimisho 25, ikiwa ni pamoja na hafla za kimataifa. "Usambazaji wa 'ICH': Vijana, elimu na maendeleo" huko Riga, Latvia (Mei 2005). ITH ilianzisha maonyesho ya '*Turathi-Hai* (Julai 2005), kwa muonekano, Ukumbi wa Umoja wa Mataifa (UN Pavilion) katika Maonyesho ya Kimataifa huko Aichi, Ujapani.

#### MIKUTANO YA KIMAENEO YA HABARI

- **Afrika Magharibi** – Dakar (Senegal), Juni 2004
- **Latini Amerika** – Paraty (Brazil), Juni 2004
- **Asia** – New Delhi (India), Septemba 2004
- **Eastern and southern Africa** – Nairobi (Kenya), Novemba 2004
- **Uropa and Kaskazini America** – Kazan (Russia), Desemba 2004
- **Mataifa ya Kiarabu** – Algiers (Algeria), Januari 2005
- **Caribbean** – Roseau (Dominica), Februari 2005

#### MIKUTANO YA KIMSINGI YA WATAALAMU

- **Jinsia na Turathi za Tamaduni Zisizogusika** – Paris, Desemba 2003
- **Kulinda muziki wa kitamaduni** – Paris, Desemba 2003
- **Makavazi na Turathi za Tamaduni Zisizogusika** – Oud-Poelgeest (Uholanzi), Aprili 2004
- **Mafunzo ya Kijamii, mila na sherehe** (matayarisho ya kawaida) – Paris, Julai 2004
- **Miundo ya Kiuvumbuzi** - Paris, Machi 2005
- **Mila za kimuziki, densi na maigizo** (matayarisho ya kawaida) – Paris, Novemba 2005
- **Kigezo cha kuteua** – Paris, Desemba 2005
- **Kuhifadhi nyaraka na Kuakibisha** – Paris, Januari 2006
- **Mila za uzungumzaji na mioneko** (matayarisho ya kawaida) – Paris, Januari 2006


© Philippe Bordas/UNESCO

*Nafasi ya tamaduni ya Sosso-Bala huko Nyagassola. Kito cha thamani kilichopatikana mnamo 2001. Sosso-Bala ni 'balofoni' iliyochezwa na wazee kutoka Guinea wa jamii ya Mandingue, wakati walipokuwa wakisindikiza utendi wa kishairi.*